# Kikao cha Tatu cha Bunge la Sita cha
# Bunge la Afrika

## SHERIA YA MFANO YA USHIRIKA YA AFRIKA

## Imeandaliwa kwa ajili ya Majadiliano ya Mkutano wa Bunge

**Juni 2024**

**Yaliyomo**

DIBAJI……………………………………………………………………………………1
1. Utangulizi………………………………………………………………………………..1
2. Uhalali wa Sheria ya Mfano ya Vyama vya Ushirika kwa …………………………...2
3. Mchakato wa Kuandaa Sheria ya Mfano …………………………………….…….3
4. Mawanda na madhumuni ya Sheria ya Mfano……………………………………..4
5. Hitimisho…………………………………………………………………………………………………………….5
6. Dibaji…………………………………………………………………………………...6
7. SEHEMU YA 1; MASHARTI YA JUMLA…………………………………………..8
8. Ibara ya 1:

## 1. Utangulizi

Sheria ya mfano ni seti ya masharti yanayojumuisha viwango bora vilivyopendekezwa kimataifa kuhusu mada maalumu ili kutumika kama kigezo au mwongozo kwa sheria za taifa zitakazopitishwa au kurekebishwa. Kwa vile sheria ya mfano ni mwongozo unaovuka mipaka ya taifa, sheria ya mfano inaweza kutumika kama ilivyo, au kurekebishwa au kupitishwa ili kuendana na mazingira mahususi. Umoja wa Afrika, kupitia vyombo vyake mbalimbali, imeweka utaratibu wa kupitisha sheria za mfano katika mambo yenye maslahi kwa Bara na watu wa Afrika kwa ujumla. Hadi sasa, sheria za mfano ambazo zimeandaliwa zinajumuisha: Sheria ya Mfano ya Usalama wa Viumbe katika Teknolojia ya Umoja wa Afrika, Sheria ya Mfano ya Haki za Jamii za Wenyeji, Wakulima na Wafugaji ya Umoja wa Afrika, na Sheria ya Mfano ya Upataji wa Taarifa katika Afrika. Pia, kuna jitihada zinazoendelea za kuandika Sheria ya Mfano ya Afrika ya Kupambana na Ugaidi na nyingine kuhusu Uridhiaji wa Mikataba. Kwa kuzingatia zoezi hili na mamlaka uliyopewa katika Ibara ya 11(3) na (7) ya Mkataba Ulioanzisha Jumuiya za Uchumi za Afrika inayohusiana na Bunge la Afrika (Mkataba wa BA) na Kanuni ya 4 (d) na (e) ya Kanuni za Uendeshaji wa BA, Bunge la Afrika pia limeandaa sheria kadhaa za mfano katika maeneo mengi, ikiwa ni pamoja na shughuli za polisi katika Afrika, ulemavu katika Afrika, usalama wa chakula na lishe na makubaliano ya utozaji kodi maradufu. Hivi karibuni, kwa kuzingatia mapendekezo ya Kamati ya Fedha, BA limekubali kuandaa sheria ya mfano ya Afrika kuhusu mfano wa shughuli za ushirika kutokana na umuhimu wake wa kuwawezesha watu kijamii na kiuchumi.

## 2. Uhalali wa Sheria ya Mfano ya Vyama vya Ushirika kwa Afrika

Moja ya malengo ya msingi yay a kuanzisha Umoja wa Nchi Huru za Afrika (OAU) ilikuwa ni kuikomboa Afrika kutoka katika utawala wa kikoloni, unyonyaji na ukandamizaji (*Ibara ya II ya Mkataba wa OAU, 1963*). Baada ya nchi zote za Afrika kupata uhuru wao (1993), nchi za Afrika zilielekeza jitihada zao katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya watu wao na Bara kwa ujumla. Mpango huu unaakisi katika Mkataba Ulioanzisha Umoja wa Afrika mwaka 2000, hususan katika Ibara 3. Moja ya njia za kufanikisha malengo ya Umoja wa Afrika ni kupitia uunganishaji wa jitihada za pamoja, vyama mbalimbali vya watu wa Afrika na serikali zao. Kwa ufupi, jitihada za pamoja zinatakiwa ili kuhakikisha matokeo ya mipango na sera za AU vinawafikia watu wa ngazi ya chini kabisa. Moja ya utaratibu muhimu ambao unaweza kuchangia katika jitihada hizi ni mfano wa ushirika wa biashara.

Umoja wa Afrika unatambua vyama vya ushirika kama asasi binafsi za biashara ambazo ni za kipekee kwa kuwa wamiliki wake wanazisimamia kidemokrasia na wananufaika nazo. Licha ya hilo, ni taasisi zinazoongozwa kwa kuzingatia thamani na zinaendeshwa kwa misingi ya kanuni, kwa kuweka mbele maslahi ya kijamii na kiuchumi ya wanachama wake. Kutokana na namna vilivyo, vyama hivyo vya ushirika ni mfano wa kupambana na umaskini na kuleta mshikamano wa kijamii. Aidha, vyama vya ushirika vinatoa fursa ya mgawo sawa wa mali kwa sababu watu wengi wanaweza kuzimiliki na kuzisimamia. Hii inawezesha zaidi ugawanyaji mkubwa wa mali na kupunguza mali hizo kurundikana katika mikono ya wachache. Kwa kufanya hivyo, vyama vya ushirika pia vinatimiza wajibu wa kupunguza tatizo la kutokuwepo usawa katika jamii, ambalo ni tatizo linaloendelea kukua duniani. Katika dunia ambapo 1% ya binadamu inadhibiti kiasi kikubwa cha mali kuliko wengine 99%, jitihada za kuondoa tofauti kati ya tajiri na maskini lazima zichukuliwe. Jukumu la vyama vya ushirika katika jambo hili lina umuhimu mkubwa sana.

Vyama vya ushirika vinatambulika kama aina ya biashara imara na endelevu kwa sababu vinaendeshwa na maadili ambayo yanalenga kukidhi mahitaji ya kijamii, kiuchumi na kiutamaduni ya wanachama wake. Kutokana na namna vilivyo, vyama vya ushirika vinaweza kuchangia katika kufanikisha dira ya UA ya “Afrika iliyoungana, yenye mafanikio na amani, inayoongozwa na watu wake wenyewe na kuwakilisha msukumo wa mabadiliko katika uwanja wa kimataifa. Vyama vya ushirika vinafaa moja kwa moja katika ajenda hii kwa kuwa vinatetea umoja, mafanikio ya kiuchumi na mshikamano. Sio hilo tu, bali vimelenga kuchangia katika utekelezaji wa Malengo

ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (Ajenda ya UN ya 2030). Hata hivyo, ili vyama vya ushirika vitimize wajibu wake ipasavyo, lazima vifanye kazi katika mazingira mazuri ambayo yanachochea ukuaji wake. Mazingira mazuri kwa kawaida yanawekwa na sheria za taifa ambazo zinaweka mifumo ya udhibiti na mambo mengine yanayohusiana na uanzishaji na uendeshaji wa vyama vya ushirika.

Ingawa ushirikiano umekuwa ni jambo la msingi katika ustaarabu na maendeleo ya Afrika, mfumo wake wa kitaasisi (yaani.vyama vya ushirika) hauna asili ya Afrika. Vyama vya ushirika vilianzishwa Afrika na watawala wa kikoloni ili kukidhi malengo mahususi ya kikoloni. Kutokana na hilo na mambo mengine, vyama vya ushirika Afrika sasa vinaendeshwa katika mazingira tofauti kisiasa, kiuchumi na kijamii. Licha ya tofauti hizo za uendeshaji, vyama vya ushirika vinapigania malengo ya pamoja na kukabiliwa na changamoto zinazokaribia kufanana. Baadhi ya changamoto zinajumuisha sheria zenye vizuizi, sheria zisizotosheleza, kuingiliwa kisiasa, wanachama wasiojali, usimamizi mbaya na matumizi madogo ya teknolojia. Katika jitihada za kutatua changamoto hizo kisheria, sheria hii ya mfano imeandaliwa ili kutoa mwongozo unaofanana kwa nchi zinapopitisha sheria mpya au kurekebisha zile zilizopo. Hata hivyo, katika nyakati tofauti, Mkutano wa Mawaziri wa Afrika - ICA umepitisha maazimio ambayo yanaeleza haja ya kuwa na sheria ya vyama vya ushirika ambayo inazingatia kanuni za vyama vya ushirika.

## 3. Mchakato wa Kuandaa Sheria ya Mfano

Katika Mkutano wa Kwanza wa Kawaida wa Bunge la Sita la Bunge la Afrika, uliofanyika Midrand, Afrika Kusini mwezi Novemba 2022, Bunge la Afrika liliazimia kuandaa sheria ya mfano ya vyama vya ushirika katika Afrika kwa kuzingatia pendekezo lililowasilishwa na Muungano wa Kimataifa wa Vyama vya Ushirika (ICA), Kanda ya Afrika (Alliance Africa). Ili kufanikisha lengo hilo, Alliance Africa, Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), kilichopo Tanzania na Sekretarieti ya Bunge la Afrika walishirikiana kwa pamoja kutoa rasimu na msaada wa kitaalamu kwa Kamati ya Fedha.

Katika kuandaa sheria ya mfano, waandishi wa sheria walichukua mawazo kutoka vyombo vya kitaifa na kimataifa , ikiwemo tamko la (ICA) kuhusu Utambulisho wa Ushirika, miongozo ya Umoja wa Mataifa inayolenga kuweka mazingira wezeshi ya uanzishaji wa ushirika, miongozo ya Sheria za Ushirika wa Shirika la Kazi Duniani (ILO), Uhimizaji wa Pendekezo la ILO la Vyama

vya Ushirika 2002 (Na. 193), Pendekezo la ILO la Vyama vya Ushirika (Nchi zinazoendelea) Pendekezo, 1966 (Na. 127), Mswada wa Vyama vya Ushirika wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa 2014, na Sheria ya Kufanana ya Vyama vya Ushirika ya OHADA, 2010. Aidha, Rasimu ya Sheria ya Mfano pia inatokana na sheria za ushirika katika nchi za Afrika na sehemu nyingine za dunia kwa madhumuni ya kukusanya taratibu nzuri, viwango bora na vipengele vinavyoibuka kuhusiana na vyama vya ushirika. Kwa kuongezea, kazi za kitaalamu zilizochapishwa kuhusu ushirika kwa ujumla na hususan sheria ya ushirika, pia zilitolewa ushauri na kuwekewa maoni mazuri ambayo yalisaidia kuiboresha rasimu hii ya Sheria ya Mfano. Zaidi ya hayo, maoni muhimu yalipatikana kutoka Kamati ya Sheria ya ICA, na ofisi ya sheria ya BA. Aidha, matokeo ya utafiti wa Uchanganuzi wa Mfumo wa Sheria wa ICA yalikuwa na manufaa katika kufuata rasimu ya Sheria ya Mfano. Rasimu ya kwanza ya Sheria ya Mfano iliwasilishwa mbele ya Kamati ya Fedha ya BA mmwezi Machi 2023, ambapo ilipata maoni ambayo yaliwezesha kuboresha rasimu na kupendekeza iwasilishwe kwa ajili ya kusoma kwa mara ya kwanza na kujadiliwa na Bunge. Mara baada ya kujadiliwa na Bunge, rasimu ya Sheria ya Mfano itaendelea kupitiwa kwa ajili ya ushauri wa kanda na/au kitaalamu, ili kukusanya michango, matakwa na matatizo ya watu na taasisi ambazo zinaweza kuwa kuwa na maslahi nayo au kuathiriwa na rasimu ya Sheria hii ya Mfano.

## 4. Mawanda na madhumuni ya Sheria ya Mfano

Kutokana na ukweli kwamba Sheria ya Mfano inatakiwa kuwa mwongozo au kigezo katika kuandaa na kupitia upya sheria za ushirika, inazungumzia tu vipengele muhimu ambavyo kwa kiasi kikubwa vinalenga kuifanya sheria ya ushirika ijikite kwa wanachama. Muundo wa sheria ya ushirika unapaswa kulenga katika kuhakikisha wanachama wa vyama vya ushirika wanapata kitu kilicho bora kutokana na sheria hiyo. Sheria ya mfano haielezi sana vipengele vya kiutaratibu kwa vile vinaweza kujumuishwa katika kanuni na taratibu na uendeshaji wa ushirika na sheria za utawala kwa kuzingatia mazingira mahususi ya taifa.

Sheria ya Mfano itashughulikia malengo ya msingi yafuatayo:

(i) Kuongoza uandaaji wa sheria mpya za ushirika na kupitia zilizopo. Kuna nchi ambazo hazina sheria ya ushirika. Sheria ya Mfano inaweza kuwa msukumo / kichocheo cha

kupitisha sheria mpya. Hata hivyo, kwa kutumia Sheria ya Mfano, sheria zilizopo zinaweza kuboreshwa ili kuakisi mahitaji na mwelekeo wa sasa.

(ii) Chombo cha ushawishi kwa ajili ya kuandaa na kupitia sheria ya ushirika. Katika kuandaa na kupitia upya sheria za taifa, mara nyingi, nchi zinaepuka kunakili 'mambo' kutoka nchi nyingine. Sheria ya Mfano itatumika na kuchukuliwa kama sharia ilyo juu ya sheria ya taifa. Kwa maana hiyo, itakuwa rahisi kwa vikundi vya ushawishi kuitumia katika kuzishawishi serikali ama kutunga sheria mpya au kupitia upya zilizopo.

(iii) Uandikaji wa taratibu nzuri. Sheria ya Mfano ni mkusanyiko wa taratibu nzuri. Kwa hiyo, itakuwa ni 'sehemu unapopata kila kitu' kwa wale wanaotaka kuchukua taratibu nzuri katika kuandaa au kupitia upya sheria za ushirika.

(iv) Sheria ya Mfano itakuwa kichocheo cha kuoanisha sheria za ushirika na utaratibu katika Afrika. Kwa kufanya hivyo, harakati za ushirika katika Afrika zitakuwa na uwezo wa muungano, uoanishaji na ushirikiano mkubwa.

## 5. Hitimisho

Vyama vya ushirika duniani kote vimekuwa vikibainishwa kama taasisi bora za kuwawezesha watu wa kipato cha chini na maskini. Vinatoa mifumo inayofaa na ya haki kwa kutafuta rasilimali kidogo kwa ajili ya kupata faida za kiuchumi na hatimae faida kubwa ya kiuchumi. Pia vinasaidia kupata huduma za kifedha, hususan maeneo ya vijijini, kwa kuwa vinatoa huduma za mikopo kwa gharama ndogo iliyo rahisi kumudu. Hata hivyo, ili vyama vya ushirika viweze kutimiza jukumu hili kikamilifu na kwa manufaa, mazingira mazuri lazima yawekwe na sheria wezeshi. Kwa misingi hiyo, sheria ya ushirika inapaswa sio tu kutambua na kulinda utambulisho wa vyama vya ushirika, bali pia itengeneze mazingira mazuri kwa ajili ya kuanzisha na kuendesha vyama vya ushirika. Rasimu hii ya Sheria ya Mfano inalenga mfumo wenye kanuni ambao unaviwezesha vyama vya ushirika kuwa taasisi hasa zinatokana na wanachama, zinazokidhi mahitaji na matamanio ya wanachama, zinachangia vizuri katika maendeleo ya taifa na bara, na kutimiza wajibu unaofaa katika kufanikisha malengo ya kijamii na ya maendeleo ya Afrika na dunia. Rasimu ya Sheria ya Mfano inalenga kuifanya sheria ya ushirika kuwalenga wanachama na inasisitiza mkabala wa 'kuona lakini siyo kufanya maamuzi ya vyama vya ushirika wakati wa kudhibiti vyama hivyo.

Sahihi………………………………………………………Afisa wa Bunge la Afrika

**DIBAJI**

**Bunge la Afrika:**

**LIKIZINGATIA** Ibara ya 17 ya Sheria Iliyoanzisha Umoja wa Afrika katika kuanzisha Bunge la Afrika ili kuhakikisha ushiriki kikamilifu wa watu wa Afrika katika maendeleo na ushirikiano wa kiuchumi wa bara;

**LIKIZINGATIA** pia Ibara ya 3 ya Mkataba Ulioanzisha Jumuiya ya Uchumi ya Kanda Inayohusiana na Bunge la Afrika, na kanuni ya 4 (a) ya Kanuni za Uendeshaji wa Bunge la Afrika, ambayo inalipa BA mamlaka ya kuwezesha utekelezaji wa sera, malengo na programu za Umoja wa Afrika na kusimamia utekelezaji wake wenye ufanisi;

**LIKIREJEA** dira ya Ajenda ya UA ya 2063, ambayo ni kuwa na Afrika iliyoungana, yenye ustawi na amani, inayoongozwa na watu wake yenyewe na kuwakilisha nguvu ya mabadiliko katika nyanja ya kimataifa;

**LIKIREJEA ZAIDI** Malengo ya Ajenda ya UA ya 2063 ambayo, pamoja na mambo mengine, yanalenga kufanikisha ukuaji wa pamoja, maendeleo endelevu, maendeleo yanayowajali watu na kuifanya Afrika imara, thabiti na iliyoungana;

**LIKITAMBUA** Pendekezo193 la ILO kuhusu Uendelezaji wa Vyama vya Ushirika ambalo linasisitiza kutafuta uwezekano wa kuandaa miongozo na kanuni za pamoja za kanda kuhusu vyama vya ushirika;

**LIKIKUMBUKA** Miongozo ya Umoja wa Mataifa unaolenga katika kujenga mazingira ya Kusaidia Maendeleo ya Vyama vya Ushirika (2001) ambayo inazitaka serikali kutengeneza mazingira ambapo vyama vya ushirika vinaweza kushiriki kwa usawa na aina nyingine za biashara, kulinda na kuendeleza uwezekano wa vyama vya ushirika wa kuwasaidia wanachama kufikia malengo yao binafsi;

**LIKIZINGATIA** Miongozo ya ILO ya Sheria za Ushirika (2016) ambayo kwa upande mmoja inawakilisha kanuni muhimu na nadharia ambazo zinapaswa kusaidia sheria za ushirika na mfumo wa kivitendo kwa ajili ya kutayarisha sheria za vyama vya ushirika kwa upande mwingine;

**LIKIZINGATIA** kupitishwa kwa Mswada wa Vyama vya Ushirika wa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 2014 ambao unatarajiwa kuwa Sheria ya Jumuiya baada ya kupitishwa na Wakuu wa Nchi za nchi wanachama;

**LIKIZINGATIA ZAIDI** kupitishwa kwa Sheria ya Pamoja ya Vyama vya Ushirika na Baraza la Mawaziri wa Shirika la Kuoanisha Sheria za Biashara katika Afrika (OHADA) mwaka 2010 na kuhusu Nchi Wanachama wa Mkataba wa Kuoainisha Sheria za Biashara barani Afrika

**LIKIREJEA** ibara ya 10 ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu ambao unampa kila mtu haki na uhuru wa kujumuika;

**LIKITAMBUA** kwamba harakati za vyama vya ushirika ni suala la kimataifa zikiongozwa na ICA, kwa kuzingatia utambulisho wa pamoja wenye misingi ya maadili na kanuni zinazotambuliwa kimataifa kama ilivyoelezwa katika Taarifa ya ICA kuhusu Utambulisho wa Ushirika;

**LIKISIKITISHWA** kwamba vyama vya ushirika katika nchi nyimgi za Afrika vinakabiliwa na changamoto ambazo zinavizuia kutimiza mahitaji ya wanachama wake wala kuchangia katika malengo ya maendeleo ya taifa na Bara;

**LIKIFAHAMU** uwezo wa vyama vya ushirika katika kupambana na umaskini katika bara kwa kuboresha maisha ya watu na kuchangia katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya taifa na bara;

**KWA MUJIBU WA** Ibara ya 11(3) na (7) ya Mkataba ulioanzisha Jumuiya ya Uchumi ya Kanda inayohusiana na Bunge la Afrika (Mkataba wa BA) na Kanuni ya 4 (d) na (e) ya kanuni za Uendeshaji wa BA ambayo inalipa BA mamlaka ya kuoanisha na kuratibu sheria na sera za Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika;

**KWA HIYO SASA,** Bunge la Afrika hapa linatunga Sheria ya Mfano ya Vuama vya Ushirika katika Afrika kama ifuatavyo:

## SEHEMU YA 1

## MASHARTI YA JUMLA

**Ibara ya 1: Kifupisho cha Sheria**

Sheria hii inaweza kunukuliwa kama "Sheria ya Mfano wa Ushirika ya Afrika"

Ibara ya 2: Mawanda ya Sheria

1. Sheria hii itahusu vyama vyote vya ushirika, sambamba na sheria zilizopo zinazohusu udhibiti wa vyama vya ushirika.
2. (2) Hakuna chochote katika Sheria hii kitakachoweza kuzuia haki ambayo tayari imetolewa chini ya sheria zilizopo za kimataifa, kikanda au kitaifa.

**Ibara ya 3: Sheria ya Msingi**

1. Sheria hii itakuwa ya msingi katika masuala yanayohusu uundaji na mpangilio wa vyama vya ushirika.
2. Pale ambapo kuna haja ya sheria mahsusi ya kusimamia aina fulani ya vyama vya ushirika, sheria hiyo itatungwa kwa misingi ya kanuni na malengo ya jumla ya sheria hii.
3. (3) Katika kutunga sheria nyingine zinazohusu vyama vya ushirika, serikali wakati wote itahakikisha kwamba utambulisho wa vyama vya ushirika unalindwa.
4. Iwapo kutatokea mgongano wowote na sheria nyingine yoyote ya vyama vya ushirika, masharti ya Sheria hii yatatumika.

**Ibara ya 4: Lengo la Sheria hii**

Sheria hii inasimamia uanzishaji, uandaaji, usimamizi, uendelezaji, uendelezaji wa vyama vya ushirika na mambo mengine yanayohusiana nayo.

**Ibara ya 5: Tafsiri**

(1) Wakati wa kutafsiri Sheria hii, itabidi kuzingatia malengo yake, katiba na sheria zozote zinazohusika za kimataifa, kikanda na za kanda ndogo.
(2) Masharti yaliyotajwa humu yatatafsiriwa ili kuhifadhi utambulisho wa ushirika na kutoa tafsiri nzuri kwa vyama vya ushirika.

**Ibara ya 6: Ufafanuzi**

Katika Sheria hii,  isipokuwa pale ambapo muktadha unaeleza vinginevyo:

***"Mkaguzi"*** ni mtu aliyesajiliwa kulingana na vigezo vinavyosimamia wahasibu na wakaguzi wa mahesabu na inajumuisha kampuni iliyofafanuliwa kwa namna hiyo, pale inapofaa na mtu mwingine yeyote aliyeidhinishwa na kanuni za ukaguzi wa vyama vya ushirika;

***"Bodi ya wakurugenzi/kamati ya uongozi/bodi"*** maana yake ni chombo kinachochaguliwa na mkutano mkuu/mkutano ili kusimamia shughuli za kila siku za chama cha ushirika kwa niaba ya wanachama;

**Mamlaka Husika**

Mamlaka Husika ina maana ya afisa wa umma au chombo ambacho kinawajibika kufanya maamuzi au kuchukua hatua kuhusu masuala mahususi yanayodhibitiwa chini ya Sheria hii.

***"Shirikisho la ushirika"*** maana yake ni shirikisho la vyama vya ushirika lililoanzishwa ili kuunganisha, kuendeleza na kuendeleza maslahi ya pamoja ya vyama vya ushirika;

***"Chama cha ushirika"*** maana yake ni chama huru cha watu walioungana kwa hiari ili kukidhi mahitaji na matamanio yao ya pamoja ya kiuchumi, kijamii na kiutamaduni, kupitia shughuli inayomilikiwa kwa pamoja na kudhibitiwa kidemokrasia.

**Sheria za ushirika** maana yake ni sheria mahususi zilizotungwa au kupitishwa ili kusimamia masuala ya vyama vya ushirika. Hii ni pamoja na sheria kuu ya kitaifa ya vyama vya ushirika, sheria ya aina mahususi ya vyama vya ushirika, au kanuni zilizowekwa chini ya sheria na sheria ndogo za ushirika.

**Sheria za vyama vya ushirika** ni sheria zinazotungwa na Serikali ili kusimamia baadhi ya mambo au shughuli za vyama vya ushirika. Hizi ni pamoja na sheria za kodi, kilimo na fedha.

**Utambulisho wa Ushirika** ni ufafanuzi, thamani na kanuni za Tamko la ICA la 1995juu ya Utambulisho wa Ushirika.

**Harakati za ushirika** ni jitihada za pamoja za vyama vya ushirika na wadau wa maendeleo ya ushirika katika ngazi ya kitaifa, kikanda au kimataifa ili kuendeleza mfumo wa biashara ya ushirika, kutetea maslahi ya vyama vya ushirika na kuchochea maendeleo ya ushirika kwa ujumla.

**Ushirika ngazi ya pili** ni mkusanyiko wa vyama vya ushirika vya msingi, wakati mwingine pia huitwa "umoja wa vyama vya ushirika".

**Ushirika wa ngazi ya tatu** ni kundi la vyama vya msingi, vyente ushirika ngazi ya pili au bila ngazi hiyo, na wakati mwingine huitwa "shirikisho".

**Shirikisho** ni kundi la vyama vyote vya ushirika na mashirika yao. Pale ambapo shirikisho linakusanya upya vyama vya ushirika vya sekta moja au vyenye shughuli sawa za kiuchumi wakati mwingine huitwa "kilele cha vyama vya ushirika".

***"Hisa ya mwanachama"*** maana yake ni mtaji unaotolewa na mwanachama wa ushirika kama sharti la kuwa mwanachama wa ushirika.

**Ufadhili** maana yake ni shughuli za kiuchumi kati ya mwanachama na ushirika katika kutekeleza azma ya ushirika.

**Mrejesho wa udhamini** maana yake ni sehemu ya ziada inayolipwa kwa mwanachama, kiasi ambacho ni sawa na uwiano wa thamani ya udhamini wake kulingana na thamani ya udhamini wa wanachama wote na ushirika wao katika kipindi maalum.

**Sheria ndogo** ni sheria tanzu zilizopitishwa na ushirika ili kudhibiti shughuli zake za kila siku.

**Mkutano mkuu** ni mkutano wa wanachama wote wa vyama vya ushirika na chombo cha juu kabisa kinachofanya maamuzi.

***"Taarifa"*** inajumuisha nyaraka zozote zilizohifadhiwa halisi au nakala, bila kujali jinsi zinavyoonekana, kama vile rekodi, barua, maelezo, maoni, ushauri, makubaliano, data, takwimu, kitabu, mchoro, plani, ramani, kielelezo, picha, sauti au picha zilizorekodiwa, na vitu vyovyote vinavyoshikika na visivyoshikika, bila kujali muundo au njia inayotumika kuwasilisha, vinavyomilikiwa au kudhibitiwa na mtunza taarifa ambaye ameombwa chini ya Sheria hii.

***"Mwanachama wa ushirika"*** maana yake mtu yeyote, halisi au chombo cha kisheria, ambaye anamiliki angalau hisa moja katika ushirika na kutokana na hisa hiyo, anapata cheti cha uanachama na haki ya angalau kura moja, kulingana na sheria ndogo za chama cha ushirika;

**Thamani ya kawaida** inamaanisha thamani ya hisa ya wanachama.

**Azimio la kawaida** ni uamuzi uliopitishwa kwenye mkutano mkuu na wanachama wengi waliohudhuria.

**Uwiano wa udhamini** maana yake ni uwiano ambao thamani ya miamala iliyofanywa na mwanachama kwenye ushirika katika kipindi maalum inabeba thamani ya miamala iliyofanywa na wanachama wote kwenye ushirika katika kipindi hicho.

**Faida** ina maana ya ziada ya mapato juu ya matumizi yanayotokana na shughuli na mtu ambaye si mwanachama wa ushirika.

***"Kutangaza"*** ni kufanya taarifa ipatikane katika njia na namna ambayo ni rahisi kupatikana kwa umma na inajumuisha kutoa nakala au kufanya taarifa ipatikane kupitia njia ya mawasiliano ya utangazaji na kielektoniki.

***"Mamlaka ya udhibiti"*** maana yake ni chombo cha serikali/umma (tume/wakala/idara) iliyoanzishwa kwa madhumuni ya kusajili na kudhibiti vyama vya ushirika, pamoja na kutoa ushauri na msaada wa kitaalamu kwa vyama vya ushirika pale inapolazimu;

***"Akiba"*** maana yake sehemu ya ziada ambayo inatengwa katika mfuko wa akiba wa fedha na isiyogawanywa kwa wanachama wa ushirika.

***"Azimio maalumu"*** maana yake ni azimio linalopitishwa katika mkutano mkuu na angalau theluthi mbili ya wanachama waliopo.

***"Kamati ya Usimamizi"*** maana yake ni Kamati ya wanachama ambayo inaweza kuundwa kwa mujibu wa katiba ya chama cha msingi, ili kufanya usimamizi wa bodi ya wakurugenzi/wajumbe wa bodi/wajumbe wa kamati ya menejimenti.

***"Ziada"*** maana yake ni kiasi cha fedha cha ziada kinachotokana na uendeshaji wa chama cha ushirika katika mwaka wa fedha.

**Ibara ya 7: Kanuni na maadili yanayoongoza Uanzishaji na Uendeshaji wa Vyama vya Ushirika**

(1) Uanzishaji na uendeshaji wa vyama vya ushirika vinapaswa kuongozwa kwa mujibu wa kanuni zifuatazo:

(i). Kuthamini

Kujitegemea, kila mmoja kubeba majukumu, demokrasia, usawa, mshikamano, uaminifu, uwazi, majukumua ya kijamii na kujali wengine

**(ii)** Kanuni

Kanuni za ushirika ni mwongozo unaofanya vyama vya ushirika kutekeleza mambo vinavyothamini.

1. **Uanachama wa hiari na wazi**

Uanachama katika ushirika ni wa hiari na uko wazi kwa watu wote ambao wanaweza kutumia vizuri huduma yake na kukubali majukumu ya uanachama, bila kujali mazingira ya kimbari, kidini, kijinsia au kiuchumi.

**2. Udhibiti wa Kidemokrasia wa Uanachama**

Vyama vya ushirika ni taasisi za kidemokrasia ziazodhibitiwa na wanachama wake, ambao wanashiriki kikamilifu katika kuweka sera na kufanya uamuzi. Wawakilishi (wakurugenzi/wadhamini) wanachaguliwa miongoni mwa wanachama na wanawajibika kwao. Katika vyama vya ushirika vya msingi, wanachama wana haki sawa za kupiga kura (mwanachama mmoja, kura moja); vyama vya ushirika katika ngazi nyingine vinaandaliwa katika namna ya kidemokrasia.

**3. Ushiriki wa Kiuchumi wa Wanachama**

Wanachama wanachangia kwa usawa na kudhibiti kidemokrasia mtaji wa ushirika wao. Angalau sehemu ya mtaji huo inabakia kuwa mali ya pamoja ya ushirika. Wanachama kwa kawaida wanapata fidia kidogo kutokana na mtaji waliochangia kama sharti la kujiunga uanachama. Wanachama wanatenga ziada kwa madhumuni yoyote au yote yafuatayo: kuendeleza ushirika; kupanga akiba; kuwanufaisha wanachama kwa uwiano katika miamala yao na ushirika; na kusaidia shughuli nyingine zinazoidhinishwa na uanachama.

**4. Kujitawala na Uhuru**

Vyama vya ushirika vinajitawala, taasisi zinazojisaidia zinazodhibitiwa na wanachama wake. Kama wanaingia katika makubaliano na taasisi nyingine, ikijumuisha serikali, au kupata mtaji kutoka vyanzo vya nje, wanafanya hivyo kwa masharti ambayo yanahakikisha udhibiti wa kidemokrasia wa wanachama na wanabakia na uhuru wa ushirika wao.

5. **Elimu, Mafunzo na Taarifa**

   Vyama vya ushirika vinawapatia wanachama elimu na mafunzo, wawakilishi waliochaguliwa (wakurugenzi/wadhamini), mameneeja na wafanyakazi ili waweze kuchangia kwa ufanisi katika maendeleo ya vyama vyao vya ushirika. Vyama vinautaarifu

umma kwa ujumla, hususan vijana na  na viongozi wanaoaminika, juu ya ushirika na manufaa yake.

### 6. Ushirikiano Miongoni mwa Vyama vya Ushirika

Vyama vya ushirika vinawatumikia wanachama wake kwa ufanisi mkubwa  na kuimarisha harakati za ushirika kwa  kufanya kazi pamoja kupitia miundo ya eneo, taifa, kanda na kimataifa.

6. **Matatizo ya Jamii**
   Vyama vya ushirika vinafanya kazi kwa ajili ya maendeleo endelevu ya jamii zao kupitia sera zilizopitishwa na wanachama **wao.**

### Ibara ya 8: Wajibu wa serikali katika maendeleo ya ushirika

(1) Wajibu mkubwa wa serikali katika maendeleo ya ushirika utakuwa ni kuwezesha sera na mfumo wa sheria kwa ajili ya kuanzisha na kuendesha vyama vya ushirika kulingana na maadili na kanuni za vyama vya ushirika.

(a) Kutayarisha sera ya maendeleo ya ushirika

(b) Kuweka taasisis zenye ufanisi za kuthibiti ushirika

(c) Kuhakikisha sheria za ushirika zinaendana na utambulisho wa ushirika na sheria za ushirika za kimataifa

(d) Kuhakikisha sheria za ushirika zinaendana na utambulisho wa ushirika

(e) Kushirikiana na harakati za ushirika na wadau wengine katika kuhamasisha maendeleo endelevu ya ushirika

**(f)** Kuhakikisha kwamba vitendo vya serikali kwa ushirika vinaendana na tunu na kanuni za ushirika.

## SEHEMU YA II

## UANZISHAJI NA MUUNDO WA VYAMA VYA USHIRIKA

### Ibara ya 9: Aina za Vyama vya Ushirika

(1) Chama cha ushirika kinaweza kuanzishwa ili kufanya biashara katika sekta yoyote ya uchumi na kushughulika na:

(a) Huduma za kifedha kama kuweka akiba na kutoa mikopo, mabenki na bima;

(b) Biashara ya ujumla na rejareja baina ya wanachama;

(c) Uzalishaji wa mazao, ununuzi, kusindika na  na kusambaza bidhaa;

(d) Uzalishaji wa viwandani na usambazaji waa bidhaa;

(e) Ujenzi wa nyumba za wanachama, na biashara ya mali isiyohamishika

(f) Ufugaji

(g) Uzalishaji wa maziwa;

(h) Uzalishaji wa mbegu

(i) Uvuvi, usindikaj na utafutaji wa masoko ya samaki na mazao mengine ya baharini;

(j) Madini, uchakataji na kutafuta masoko ya bidhaa za madini;

(k) Huduma za afya;

(l) Huduma za TEHAMA;

(m) Huduma za kitaalam, hususan uhasibu, sheria na uhandisi;

(n) Mitindo, ubunifu na huduma husika;

(o) Huduma za kifedha;

(p) Huduma za usafi.

### Ibara ya 10: Uanzishaji wa ushirika

(1) Ushirika utaanzishwa kufuatana na mahitaji ya kiuchumi ya wanachama wake na tunu na kanuni za ushirika.

(2) Bila ya kuathiri mahitaji ya aina maalum, aina au madaraja ya vyama vya ushirika, mahitaji muhimu ya usajili wa ushirika yatajumuisha:

(a) Ripoti ya tathmini ya uwezo;

(b) Sheria ndogo zinazopendekezwa;

(c) Orodha ya wanachama waanzilishi; na

(d) Azimio la kuunda ushirika ikijumuisha majina ya wawakilishi walioteuliwa.

(3) Inapobidi ushirika uanzishwe, wanachama waasisi au wawakilishi wao walioteuliwa, watawasilisha kwa mamlaka husika vitu vinavyohitajjika na kuainishwa kwenye ibara ndogo (2)

(4) Baada ya kupokea maombi ya usajili mamlaka husikka itakiri kupokea mara moja na itaamua juu ya maombi ndani ya muda usiozidi siku thelathini (30).

(5) Pale ambapo maombi ya usajili yanakubaliwa, mamlaka husika itatoa cheti cha usajili kilichotiwa saini kwa chama ambacho kitakuwa ni ushahidi tosha kwamba chama kilichotajwa humo kimesajiliwa ipasavyo.

(6) Endapo maombi ya usajili hayakidhi mahitaji yaliyoainishwa katika ibara ndogo ya 2, Mamlaka yenye uwezo itayakataa na kutoa sababu za kukataliwa huko.

(7) Pale ambapo waombaji hawajaridhika na kukataliwa, wanaweza kutuma maombi ya mapitio ya kiutawala na au ya kimahakama.

**Ibara ya 11: Ofisi Iliyosajiliwa**

(1) Chama cha ushirika kitakuwa na ofisi iliyosajiliwa ndani ya nchi.

(2) Mabadiliko yoyote kuhusu eneo la ofisi iliyosajiliwa yatawasilishwa kwa Mamlaka husika ndani ya muda wa siku thelathini (30).

**Ibara ya 12: Hadhi ya Kisheria ya Ushirika**

Baada ya kusajiliwa, chama cha ushirika kitakuwa shirika kwa jina ambalo kimesajiliwa, cha kudumu, chenye muhuri, na chenye uwezo wa kuhifadhi mali inayohamishika na isiyohamishika ya aina yoyote, kuingia mikataba, kushtaki na kushtakiwa. na kufanya mambo yote muhimu kwa madhumuni ya, au kwa mujibu wa Sheria hii na sheria ndogo zake.

**Ibara ya 13: Utoaji wa Jina**

(1) Kila ushirika utajumuisha neno “ushirika” katika jina lake na kila shirikisho la vyama vya ushirika na chama kikuu kitajumuisha neno “shirikisho” au “kikuu” kwa mfuatano huo katika jina lake.

(2) Hakuna ushirika wala shirikisho la vyama vya ushirika litakalotumia jina lolote linalofanana au kupotosha kufanana na ushirika mwingine.

(3) Hakuna ushirika utakaotumia jina la nchi au chombo chake chochote au shirika la kimataifa.

(4) Vyama vya ushirika na mashirikisho yanaweza kuhimiza matumizi ya utambulisho wa jina la ushirika duniani linalojulikana sana na linalosambazwa na kuenezwa na ICA.

(5) Hakuna chombo zaidi ya ushirika uliosajiliwa chini ya Sheria hii ambao;

(a) Utajisimamia wenyewe kama kufanya biashara kama chama cha ushirika kilichosajiliwa.

(b) Utatumia au kuidhinisha matumizi ya maneno ‘‘ushirika’, ‘‘co-op’’, ‘‘cooperative limited’’, ‘‘co-operative ltd’’, au ‘‘co-op ltd’’ au “chama cha ushirika” kama sehemu ya jina lake.

(c) Mtu anayekiuka vifungu hapo juu anatenda kosa na akitiwa hatiani, atastahili kulipa faini.

**Ibara ya 14: Uanachama wa chama cha ushirika**

(1) Uanachama wa chama cha ushirika uko wazi bila ya ubaguzi kwa watu wote wanaoweza kutumia huduma za ushirika na walio tayari kukubali majukumu ya uanachama.

(2) Mtu atakuwa mwanachama wa chama cha ushirika ikiwa:

(a) Ametimiza umri wa miaka 18;

(b) Aliomba uanachama kwa hiari;

(c) Amekbaliwa na mkutano mkuu; na

(d) Amejisajili na kupataa idadi ya chini ya hisa za uanachama kama ilivyoainishwa katika sheria ndogo.

(3) Mtu mwenye umri chini ya miaka kumi na minane (18) anaweza kupewa uanachama wa chama cha ushirika kwa sharti kwamba hatapangiwa majukumu ambayo yanapaswa kutekelezwa na watu wenye umri unaotakiwa.

**Ibara ya 15: Haki ya Wanachama**

(1) Mwanachama wa chama kikuu cha ushirika ana haki ya:

(a) Kushiriki katika kufanya maamuzi kwa mujibu wa sheria ndogo;

(b) Kupokea sehemu ya faida ya ushirika;

(c) Kupokea sehemu ya ziada ya ushirika;

(d) Kusikilizwa katika masuala yanayohusu uanachama wao;

(e) Kupokea elimu, mafunzo na taarifa;

(f) Kuwachagua viongozi;

(g) Kuchaguliwa kuwa kiongozi;

(h) Kushiriki katika mikutano mikuu;

(i) Kukagua vitabu na kumbukumbu;

(j) Kuitisha mkutano mkuu kwa kuzingatia sheria ndogo;

(k) Kulipwa fudia sawa na malipo ya thamani ya kawaida ya hisa zilizolipwa baada ya kujiondoa uanachama;

(l) Kupata mgawo wa kiasi chochote kilichobaki baada ya kufutwa kwa ushirika isipokuwa mfuko wa hifadhi;

(m) Kuteua mnufaika;

(n) Kuitisha uchunguzi kuhusu masuala ya ushirika kwa mujibu wa sheria ndogo.

(2) Haki maalum zaidi za wanachama zinaweza kutolewa katika sheria ndogo ili kuakisi aina mahususi, aina au shughuli za ushirika.

**Ibara ya 16: Wajibu wa Mwanachama**

Mwanachama wa chama cha msingi cha ushirika anawajibika:

(a) Kushiriki katika shughuli za ushirika na/ au atakavyotakiwa na sheria ndogo au azimio la mkutanao mkuu;
(b) Kuheshimu sheria ndogo na maazimio yaa mkutano mkuu;
(c) Kutoa taarifa juu ya mgongano wa maslahi;
(d) Kuepuka mwenendo na /au kutotoa taarifa juu ya kitu kinachoweza maslahiya chama chake;
(e) Kulipa bei ya hisa za uanachama zinazotakiwa na ada zingine zozote kama ilivyo kwenye sheria ndogo;
(f) Kuwajibisha viongozi wao;
(g) Kuheshimu kwa uaminifu masharti ya mkataba wowote alioingia na ushirika;
(h) Kulinda mali za ushirika;
(i) Kuheshimu wajibu wowote kama inavyoainishwa kwenye sheria ndogo, hususanili kuakisi aina mahsusi au sahughuli za ushirika;
(j) Kutekeleza lolote ambalo ni lazima katika kufikia malengo ya ushirika.

**Ibara ya 17: Vizuizi vya Uanachama**

(1) Hakuna ushirika utakaokataa ombi la mtu kujiunga na ushirika kama mwanachama bila ya uhalali wa kisheria.

**Ibara ya 18: Kusitishwa kwa uanachama**

Yafuatayo yatasababisha kusitishwa kwa uanachama:
(1) Kujiondoa kwa hiari;
(2) Kufukuzwa;
(3) Kifo;
(4) Kufutwa kwa ushirika;a na
(5) Kupoteza stahiki kwa sababu ya kupoteza dhamana ya pamoja au mambo mengine.

**Ibara ya 19: Kuondoka kwenye uanachama**

(1) Mwanachama wa chama cha ushirika anaweza kujiondoa kwenye ushirika baada ya kutimiza majukumu yake ya mwanachama anayodaiwa.
(2) Sheria ndogo za ushirika zitaweka utaratibu wa kujitoa.

**Ibara ya 20: Kufukuzwa**
(1) Mwanachama wa chama cha ushirika anaweza kufukuzwa ikiwa:
(a) Ameshindwa kutimiza wajibu wake;
(b) Sababu nyingine yoyote iliyoainishwa katika sheria ndogo.
(2) Pale ambapo chama cha ushirika kinakusudia kumfukuza mwanachama kitamjulisha sababu ya kumfukuza uanachama na kufuata utaratibu kama ilivyoelezwa katika sheria ndogo.

**Ibara ya 21: Haki ya mwanachama kukata rufaa**

(1) Mwanachama aliyefukuzwa atakuwa na haki ya kukata rufaa baada ya kushindwa kwa taratibu za utatuzi wa migogoro ya ndani ya chama.

(2) Haki ya kukata rufaa itatekelezwa mbele ya mamlaka husikaya kiutawala na/au mahakama.

**Ibara ya 22: Haki ya Kudai Fidia Mwanachama anayeondoka**

(1) Mwanachama anayeondoka kwenye chama ana haaki ya kudai fidia ya hisa zake kwa thamani ya wakati huo.
(2) Fidia ya hisa itafanyika baada ya mwanachama ametimiza mashati ya kifedha ayodaiwa.
**(3)** Hisa za mwanachama zisipodaiwa ndani ya mwaka mmoja zitawekwa kwenye mfuko wa akiba.

## SEHEMU YA III
## KUUNGANA KWA VYAMA VYA USHIRIKA

**Ibara ya 23: Muunganisho wa wima**

(1) Katika kutekeleza kanuni ya ushirikiano miongoni mwa vyama vya ushirika, vyama vya ushirika vinaweza kuunganishwa kiwima au kimlalo.

(2) Vyama vya ushirika vya msingi vinaweza kuunganishwa na vyama vya ushirika ngazi ya pili.

(3) Vyama vya ushirika ngazi ya pili vinaweza kuungana na kuunda ushirika wa juu zaidi.

(4) Shirikisho la vyama vyote vya ushirika linaweza kuundwa katika ngazi ya kitaifa.

**Ibara ya 24: Muunganisho wa mlalo**

(1) Vyama vya ushirika vinaweza kuunda miundo mlalo kama vile biashara za pamoja na ubia ili kutekeleza miradi ya pamoja ya kiuchumi.

(2) Vyama vya ushirika vinaweza kuunda miundo jumuishi ambayo hurahisisha ugavi wa vifaa na huduma kama vile uuzaji na mikopo.

## SEHEMU YA IV
## UENDESHAJI WA VYAMA VYA USHIRIKA

**Ibara ya 25:** Vyombo vya uendeshaji

Muundo wa uendeshaji wa ushirika utajumuisha:

(i) Mkutano Mkuu

(ii) Bodi

(iii) Usimamizi (watumishi)

**Ibara ya 26: Mkutano Mkuu**

(1) Chama cha ushirika kitakuwa na mkutano mkuu utakaojumuisha wanachama wote na kitakuwa chombo cha juu zaidi cha ushirika cha kufanya maamuzi.

(2) Mkutano Mkuu utaitishwa kama ifuatavyo:

(a) Mkutano Mkuu wa Kawaida ambao utafanyika angalau mara moja kwa mwaka kwa mujibu wa sheria ndogo; na

(b) Mkutano Mkuu Maalum utakaoitishwa kwa sababu maalum kama itakavyoainishwa na sheria ndogo.

(3) Mkutano Mkuu wa Kawaida utaitishwa na kuongozwa na Mwenyekiti wa Bodi. Mwenyekiti asipokuwepo, au hawezi kuongoza mkutano, makamu mwenyekiti au mtu mwingine yeyote aliyeteuliwa na mkutano ndiye atakayeongoza.

(4) Wanachama watataarifiwa kuhusu vipengele vya ajenda, tarehe, muda na mahali pa mkutano mkuu kwa mujibu wa sheria ndogo.

(5) Theluthi moja ya wanachama wanaweza kuomba kwa taarifa ya maandishi kwa Mwenyekiti kufanyika kwa mkutano mkuu maalum. Ombi litatoa motisha na maelezo ya mambo yatakayojadiliwa katika mkutano mkuu maalum unaopendekezwa. Mwenyekiti ataitisha kikao hicho ambacho kitajadili mambo yaliyoainishwa katika ombi hilo.

(6) Endapo mwenyekiti atashindwa kuitisha kikao ndani ya siku kumi na tano baada ya kupokea ombi hilo, wajumbe wanaweza kuomba mamlaka husika kuitisha kikao.

**Ibara ya 27: Majukumu ya Mkutano Mkuu**

(1) Majukumu makuu ya Mkutano Mkuu yatakuwa:

(1) Kupitia na kuidhinisha marekebisho ya sheria ndogo;
(2) Kuamua juu ya kuunganisha, kugawanya na kufutwa kwa ushirika
(3) Kupitia na kuidhinisha kumbukumbu za mkutano mkuu uliopita;
(4) Kupitia ripoti za bodi au kamati;
(5) Kupitia na kuidhinisha akaunti zilizokaguliwa;
(6) Kuamua namna ya kugawana au kuwekeza ziada iliyopatikana;
(7) Kuamua ikibidi, kikomo cha juu cha kukopa cha chama cha ushirika;
(8) Kuchagua mkaguzi wa mahesabu kwa mwaka unaofuata;
(9) Kuidhinisha ununuaji na uuzaji wa mali;
(10) Kudahili, kusimamisha na kufukuza wanachama;
(11) Kuchagua au kusimamisha au kuwaondoa wajumbe wa bodi na wajumbe wa kamati za kudumu;
(12) Kuamua uanachama wa ushirika kwenye vyombo vingine;
(13) Kupitisha bajeti ya mwaka, mipango ya biashara na mipango mkakati;
(14) Kuunda kamati za mudda na kuainisha majukumu yake; na

(15) Kujadili shughuli zingine zozote za ushirika ambazo notisi yake imetolewa kwa wanachama, kufuatana na sheria ndogo za chama cha ushirika.

**Ibara ya 28: Maamuzi ya Mkutano Mkuu**

(1) Mkutano Mkuu utaamua kuhusu mambo chini ya ibara ya 27(1) kupitia azimio lililopitishwa na wajumbe wengi waliohudhuria na kupiga kura.

(2) Bila ya kujali ibara ya (1) hapo juu, azimio la mkutano mkuu kuhusu mambo yaliyoorodheshwa chini ya ibara ya 27(a) na (b) litapitishwa kwa azimio maalum, ila kwa vipengele (a) na (b) ambavyo vitahitaji

(1) Azimio kuhusu mambo chini ya kifungu cha 25 (1) litapitishwa kwa kuhudhuriwa na wajumbe walio wengi na kwa kura ya "ndiyo" ya wajumbe wasiopungua theluthi mbili waliohudhuria kikao, wakati azimio kuhusu mambo mengine litapitishwa kwa mahudhurio ya wengi wa wanachama wote na kwa kura ya "ndiyo" ya wajumbe walio wengi waliopo kwenye mkutano.

(2) Kumbukumbu za mkutano mkuu zitachukuliwa na mtu mahsusialiyeteuliwa na mwenyekiti kwa ajili hiyo katika mkutano mkuu. Yaliyomo katika kumbukumbu yatajumuisha shughuli na matokeo ya mkutano, ambapo mwenyekiti na angalau 25% ya kamati ya usimamizi au bodi ya wakurugenzi waliopo, wataweka mihuri au saini zao.

**Ibara ya 29: Wawakilishi katika Mkutano Mkuu**

(1) Chama cha ushirika kinaweza katika sheria ndogo zake kuanzisha mkutano mkuu wa wawakilishi kama mbadala wa mkutano mkuu wa wanachama wote.

(2) Mkutano mkuu wa wawakilishi utajumuisha wawakilishi waliochaguliwa kutoka miongoni mwa wanachama katika mgawo usio chini ya 1:50 wajumbe, ambapo 1 ni mwakilishi aliyechaguliwa;

(3) Hakuna mwakilishi atakayeidhinisha wakala wake kutekeleza haki yake ya kupiga kura kuhusu azimio au uchaguzi.

(4) Mambo muhimu ya uendeshaji wa mkutano mkuu wa wawakilishi, kama vile muda wa uwakilisshi, mbinu za uchaguzi na sifa za wawakilishi, yataainishwa na sheria ndogo.

(5) Masharti kuhusu mkutano mkuu yatatumika *mutatis mutandis* kwa mkutano mkuu wa wawakilishi, na neno "mjumbe" litafafanuliwa kama "mjumbe mwakilishi" katika hali kama hizo, mradi tu mkutano mkuu wa wawakilishi usipitishe azimio lolote kuhusu masuala yanayohusu kuunganishwa, mgawanyiko na kuvunjwa kwa ushirika.

## SEHEMU YA IV

## FEDHA ZA USHIRIKA

**Ibara ya 30**: Vyanzo vya mtaji

(1) Ada ya uanachama Fedha za chama cha ushirika zinaweza kujumuisha:

(a) usajili wa uanachama inapohitajika;

(b) hisa za wanachama;

(c) amana na akiba za wanachama;

(d) mikopo;

(e) ada au tozo zilizotajwa katika sheria ndogo; na

(f) Chanzo kingine chochote halali.

**Ibara ya 31: Dhima ya Wanachama**

(1) Mwanachama atachangia angalau hisa moja, kama ilivyoainishwa na Sheria Ndogo, na mwanachama anaweza kutoa mchango wake hali ikibidi.

(2) Idadi ya hisa ya kuchangia kwa kila mwanachama haitazidi asilimia 20 ya jumla ya hisa za kuchangia.

(3) Mchango wa wanachama kwenye ushirika utatumika kufidia madai dhidi ya mwanachama ndani ya ushirika.

(4) Deni la mwanachama halitazidi kiasi cha michango aliyochanga.

**Kifungu cha 32: Haki za kupiga kura**

(1) Kila mwanachama atapiga kura moja kwenye azimio au uchaguzi, bila kujali idadi ya hisa zake alizochangia. Katika sehemu hii, hakuna kinachokataza kupiga kura zaidi ya mara moja au kupiga kura za uwakilishi kwenye vyama vikuu.

(2) Mwanachama anaweza kutumia haki ya kupiga kura kwenye azimio au uchaguzi, kwa kutumia mwakilishi. Katika hali hiyo, itatambuliwa kwamba mwanachama alihudhuria mkutano.

(3) Mwakilishi, chini ya kifungu 17(2) atakuwa mwanachama mwingine au mwanafamilia anayeishi na mwanachama (mke au mume wa mwanachama, ndugu wa damu kwa mfano, mtoto/mjukuu, kitukuu au ndugu wa kuzaliwa au mke / mume wa mtoto, mjukuu, kitukuu au ndugu wa kuzaliwa naye, na mwakilishi wa mwanachama atakuwa mmoja tu.

(4) Mwakilisahi chini ya kifungu 17(2) atawasilisha kwa ushirika waraka unaothibitisha kwamba yeye ni mwakilishi, kufuatana na sheria ndogo.

**Ibara ya 33 Sheria au Sheria Ndogo**

(1) Sheria ndogo ni msingi wa ushirikiano wa wanachama wa ushirika na zinapaswa kuakisi mahitaji na matamanio ya wanachama, wakati huo huo zikihakikisha usalama wa utambulisho, kwa mujibu wa kifungu namba 5 cha Sheria hii.

2. Nakala ya sheria ndogo itawasilishwa kwenye mkutano mkuu maalumu ulioitishwa kwa ajili ya ajenda ya sheria ndogo, kwenye ofisi ya chama ilikosajiliwa. Wanachama wenyewe watahudhuria mkutano au kushiriki kwa njia zingine pamoja na kwa kielektroniki.

3. Sheria ndogo za ushirika zinahusu:
   (a) Malengo ya ushirika;
   (b) Jina, jina la biashara na kifupisho (kama kipo) na mahali pa ofisi;
   (c) Aina ya ushirika, sekta ya shughuli na kitu kinachowaunganisha wanachama;
   (d) Sifa za wanachama;
   (e) Udahili, kujitoa na kufukuzwa kwa mwanachama;
   (f) Mkutano Mkuu wa Mwaka na mikutano mingine lazima ya ushirika;
   (g) Kamati ya Uutawa /Uendeshaji au Bodi ya Wakurugenzi na wajibu wao; Haki na Wajibu; idadi ya chini kabisa na juu kabisa ya wanachama; muda wa bodi na wa wateuliwa wa bodi (kama ipo) na maelezo ya uteuzi huo;
   (h) Thamani ya hisa inayochangiwa kwa fedha taslimu au mali, njia na muda wa malipo ya michango, na kuweka kikomo cha idadi ya hisa kwa kila mwanachama;
   (i) Haki na wajibu wa wanachama;

(j) Ugawaji wa ziada na kuziba hasara;
(k) Njia ya kugawa na kutumia akiba;
(l) Ukaguzi wa mahesabu
(m) Baraza linalojiendesha lenye asilimia 5 ya jumla ya wanachama wa vyama vya ushirika, lililoundwa kwa hiari au kwa namna iliyoshauriwa na mamlaka husika, kusimamia na kufuatilia utendaji kazi wa kamati ya usimamizi ya bodi ya wakurugenzi, na muda wa ya muda wake;
(n) Kanuni za maadili kwa viongozi na menejimenti;
(o) Misingi/nguzo za utawala bora;
(p) Kuvunja na kuhamisha michango;
(q) Ufafanuzi juu ya utambulisho wa vyama vya ushirika na masharti ya kuhakikisha usawa wa kijinsia, ushirikishwaji na kujali mazingira; na
(r) Mambo mengine muhimu kwa uendeshaji wa mkutano mkuu na bodi ya wakurugenzi.
(s) Utaratibu wa utatuzi wa migogoro;
(t) Taratibu za kujidhibiti; na
(u) Uwajibikaji wa wanachama.

**Ibara ya 34: Kamati/Bodi ya Usimamizi**

(1) Chama cha ushirika kitakuwa na Bodi ya Wakurugenzi iliyochaguliwa kidemokrasia, ambayo itajumuisha mwenyekiti na wakurugenzi.
(2) Inapobidi bodi inaweza kualika kwa muda mfupi, mtaalam / wataalam kutoa mwongozo na msaada katika mikutano yake.
(3) Pale inapohitajika na kwa kuzingatia sheria ndogo, uundaji wa bodi uitaangazia tofauti za wanachama ikijumuisha jinsia na umri ili kuhakikisha ushirikishwaji.
(4) Mwenyekiti ataitisha vikao na kuviongoza kwa mujibu wa Sheria Ndogo.
(5) Chama cha ushirika kinaweza kuchagua kutokuwa na bodi ya wakurugenzi iwapo kitakuwa na wanachama 10 (kumi) au chini ya hapo. Chaguo kama hilo litafanywa na vyama vya ushirika kupitia azimio la mkutano mkuu.

**Ibara ya 35: Majukumu mengine ya Wajumbe wa Bodi**
(1) Kuweka hesabu na rekodi sahihi ya mali na madeni ya ushirika;
(2) Sikiliza ripoti za malipo na ripoti za maendeleo ya maafisa waliopewa majukumu maalum, hasa Mwenyekiti, Meneja na Mweka Hazina;
(3) Kuwasilisha kwenye Mkutano Mkuu wa Mwaka ripoti ya menejimenti pamoja na mahesabu yaliyokaguliwa na kuidhinishwa ipasavyo;
(4) Kuwasilisha kwenye Mkutano Mkuu wa Mwaka mpango kazi na bajeti ya mwaka ujao wa fedha kwa ajili ya kuidhinishwa;
(5) Kuwasaidia watu wote walioidhinishwa kukagua hesabu za ushirika;
(6) Kuchukua hatua zote muhimu ili kulinda fedha, mali, hisa na mali ya ushirika;
(7) Kuhakikisha kwamba pesa zilizokopwa hazizidi kiwango kilichowekwa na Mkutano Mkuu;
(8) Teua kamati ndogo ndogo pale ambapo Mkutano Mkuu umeidhinisha kufanya hivyo;
(9) Kutekeleza maamuzi yote yaliyochukuliwa na Mkutano Mkuu;
(10) Kutekeleza majukumu mengine kama yalivyoidhinishwa, ili kukuza shughuli za ushirika.

**Ibara ya 36: Mwaka wa Fedha**
(1) Mwaka wa fedha wa chama cha ushirika utabainishwa na sheria ndogo.
(2) Hesabu za Ushirika zitagawanywa katika akaunti za jumla na akaunti maalum, na sekta ya biashara kwa kila akaunti itaelezwa na sheria ndogo.

**Ibara ya 37: Mipango ya Biashara, Bajeti ya Mapato na Matumizi na Shughuli za Biashara**

(1) Chama cha ushirika, kupitia bodi yake, kitatayarisha mpango wa biashara na bajeti ya mapato na matumizi kwa kila mwaka wa fedha na kitawasilisha kwenye mkutano mkuu kwa ajili ya kuidhinishwa.
(2) Ushirika utaainisha kwa uhuru shughuli zake za kibiashara zinazohitajika ili kutimiza malengo yake ya kuanzishwa na sheria ndogo zake, lakini shughuli zifuatazo za biashara zitajumuishwa humo.
(3) Programu za ushauri nasaha, elimu, mafunzo ya wanachama na wafanyakazi pamoja na wanachama wa maeneo hatarishi katika jamii na kutoa taarifa kuhusu vyama vya ushirika na pia mada muhimu kama vile hali ya hewa, haki za binadamu, usawa wa kijinsia n.k. yao.
(4) Biashara na shughuli zinazohusiana na ushirikiano baina ya vyama vya ushirika, ikijumuisha ushirikiano wa kimataifa kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa fedha kwa vyama vya ushirika, biashara ya ndani na mipakani n.k, pamoja na kushirikiana na vyama vingine vya ushirika katika masuala yanayohusu uanzishaji wa taasisi na taratibu za kusaidia na kuwezesha biashara kama vile vyombo vya ushirika wa biashara na biashara kwa ujumla.

**Ibara ya 38: Uwazi wa Uendeshaji**
(1) Chama cha ushirika kitaweka wazi mambo yafuatayo kwa wanachama na mamlaka za kitaifa:
(a) Sheria Ndogo na mchakato wa kutunga sheria ndogo;
(b) Kumbukumbu za mikutano mikuu au mikutano ya bodi ya wakurugenzi;
(c) Orodha ya wanachama wake;
(d) Vitabu vya mahesabu; na
(e) Mambo mengine yaliyowekwa kwenye sheria ndogo.
(2) Ushirika utaweka nyaraka zake katika makao yake makuu ya biashara.

**Ibara ya 39: Hifadhi za Kisheria na Hiari**
(1) Chama cha ushirika kinapokuwa na ziada baada ya kukamilika kwa hesabu za mwaka wa fedha, kitatenga si chini ya asilimia 10 ya ziada (hapa inajulikana kama "hifadhi ya kisheria") hadi kiasi hicho kifikie mara tatu ya jumla ya fedha. za michango iliyolipwa hadi mwisho wa mwaka wa fedha husika.
(2) Ushirika unaweza kutenga akiba ya biashara na akiba nyinginezo (hapa zitajulikana kama "hifadhi za hiari"), kama ilivyoainishwa na sheria ndogo.
(3) Hakuna ushirika utakaotumia hifadhi ya kisheria isipokuwa kwa idhini ya mamlaka husika kwa mujibu wa kifungu cha 14, hifadhi ya kisheria imetengwa kwa ajili ya kuziba hasara au pale chama cha ushirika kinapovunjwa.

**Ibara ya 40: Fidia kwa Hasara na Ugawaji wa Ziada**

(1) Wakati chama cha ushirika kimepata hasara baada ya kukamilika kwa hesabu za mwaka wa fedha (ikimaanisha hasara kwa muda), kitatumia fedha zilizobaki kutoka mwaka mwingine, akiba ya hiari, na kwa idhini ya mamlaka husika, hifadhi ya kisheria kwa ajili ya kuziba hasara hiyo kwa utaratibu uliotajwa hapo juu, lakini itabeba salio la hasara hiyo hadi mwaka wa fedha unaofuata, ikiwa salio litasalia baada ya kulipa hasara.

(2) Ushirika unaweza kugawa ziada kwa wanachama, kama ilivyoainishwa na sheria ndogo, baada ya kuchukua fedha za kuziba pengo la hasara na kuweka kando hifadhi ya kisheria na akiba ya hiari.

(3) Chama cha ushirika kinapogawa ziada, mgao wa mapato kutokana na matumizi ya biashara ya ushirika hautapungua asilimia 50 ya jumla ya gawio, lakini gawio la michango iliyolipwa haitazidi asilimia 10 ya michango iliyolipwa.

**Ibara ya 41 : Kuungana na Kugawanya kwa Vyama**

(1) Ushirika unaweza kuungana na chama kingine au kujigawa baada ya mkutano mkuu kuidhinisha azimio husika, baada ya kutayarisha mkataba wa kuungana au mpango wa kujigawa.

(2) Vyama vya ushirika vinapoungana, chama kinachobaki kitawasilisha ripoti juu ya muungano; chama kinachoanzishwa baada ya kugawana kitawasilisha ripoti kwa mamlaka husika na ushirika unaofutwa baada ya vyama kuungana utawasilisha ripoti ya kufutwa kwa mamlaka husika iliyo na mamlaka juu ya ofisi yake kuu.

(3) Chama kinachobaki au kuanzishwa upya baada ya kuungana au kugawanya kitarithi haki na majukumu ya chama kilichofutwa.

**(4)** Chama chochote hakitaruhusiwa kuungana na chombo cha kisheria au ushirika isipokuwa kwa mujibu wa Sheria hii, au kumegwa na kuwa chombo cha kisheria, au ushirika isipokuwa kwa mujibu wa Sheria hii.

**Ibara ya 42: Kufutwa kwa Ushirika**

(1) Chama cha ushirika kitafutwa iwapo mojawapo ya matukio yafuatayo yanatokea:

(a) Wakati tukio lililotajwa kama sababu ya kuvunjwa kwenye sheria ndogo linapotokea.

(b) Mkutano mkuu unapoazimia kuuvunja kwa msingi unaokubalika ambao umearifiwa kwa mamlaka husika.

(c) Inapounganishwa, kugawanywa, au kufilisika.

(2) Pale ambapo chama cha ushirika kimevunjwa, mfilisi ataripoti kufutwa kwake ndani ya siku 14 baada ya kushika madaraka yake kama mfilisi, kwa mamlaka husika ambayo chama hicho kimeripoti kuanzishwa kwake.

**Ibara ya 43: Uteuzi wa Wafilisi**

(1) Chama cha ushirika kinapofutwa, mamlaka ya serikali inayohusika na vyama vya ushirika itateua mfilisi mwenye sifa.

(2) Mfilisi atakagua hali ya sasa ya mali ya ushirika bila kuchelewa baada ya kuteuliwa, kutayarisha orodha ya mali na mizania, kuamua mbinu za uondoaji wa mali, na kupata kibali kutoka kwa mkutano mkuu.

(3) Masuala ya kiutawala ya kufilisi yanapokamilika, mfilisi atatayarisha ripoti ya ukamilishaji wa hesabu bila kuchelewa na atapata kibali kutoka kwa mkutano mkuu.

(4) Iwapo chama cha ushirika kitashindwa kufanya mkutano mkuu hata baada ya kuitisha mkutano mkuu angalau mara mbili katika kesi zilizo chini ya kifungu cha 44 (2) na 44 (3), itachukuliwa

kuwa mkutano mkuu umeidhinisha masuala, hata pale ambapo chini ya theluthi mbili ya wajumbe waliopo kwenye mkutano wanaidhinisha

.

**Ibara ya 44: Mali ya Yaliyobaki**

(1) Pale ambapo chama cha ushirika kimefutwa na mali ya imebaki baada ya ulipaji wa madeni, ushirika utaondoa mali hiyo, kama ilivyoainishwa na kanuni za chama/sheria ndogo/kanuni.

(2) Bila ya kujali aya ya 1 ya kifungu hiki chama cha ushirika kinaweza kutoa mapato yake yaliyobakia kama msaada kwa kwa shirikisho la vyama vya ushirika au ushirika mwingine, kama ilivyoainishwa na sheria ndogo.

**Ibara ya 45: Usajili wa Mabadiliko**

(1) Endapo mabadiliko yoyote yatafanywa kuhusu masuala ya usajili wa wa ushirika unaoanzishwa, ushirika utawasilisha maombi ya usajili kwa mamlaka husika au ofisi za usajili zilizopo kwenye ya eneo lake kuu la biashara na ofisi ya tawi lake ndani ya siku 21.

(2) Bila ya kujali chochote kilichomo katika kifungu cha 46 (1), usajili wa mabadiliko yoyote ya masuala yanayohusu usajili utapatikana ndani ya miezi mitatu baada ya mwaka wa fedha kuisha.

(3) Wakati wa kusajili wa mabadiliko yoyote chini ya vifungu vya 46 (1) na 46 (2) mwenyekiti wa chama cha ushirika kinachohusika ndiye atakuwa mwombaji.

(4) Maombi ya usajili chini ya kifungu cha 46 (3) yataambatanishwa na nyaraka zinazothibitisha mabadiliko katika suala husika lililosajiliwa.

(5) Maombi ya usajili wa mabadiliko yoyote kutokana na kupungua kwa mtaji, muunganisho au mgawanyo yataambatanishwa na nyaraka zote zifuatazo:

(a) Nyaraka chini ya kifungu cha 46 (4).

(b) Nyaraka zinazothibitisha kwamba notisi ya umma au notisi ya uhakiki imetolewa;

(c) Hati inayothibitisha kuwa madeni yamelipwa kwa wadai waliowasilisha pingamizi au kwamba dhamana iliyotolewa kwa wadai hao.

**Ibara ya 46: Kodi za vyama vya ushirika**

(1) Katika kutoza kodi vyama vya ushirika, mambo yafuatayo yatazingatiwa:

(a) tofauti kati ya faida na ziada;

(b) sababu za malipo ya ufadhili kwa wanachama;

(c) madhumuni ya fedha za akiba katika vyama vya ushirika;

(d) uhamasishaji wa vyama vya ushirika, hasa uhusiano kati ya jamii za msingi, jumuiya za ngazi za chini na za juu, jumuiya za elimu ya juu na shirikisho;

(e) aaina ya biashara ya ushirika;

(f) ukubwa wa biashara ya ushirika; na

(g) eneo ambapo ushirika upo.

(2) Waziri anayehusika na kodi au ofisa mwingine yeyote wa umma anayehusika, anaweza kusamehe vyama vya ushirika:

(a) kodi ya ushirika kwa mashirika ambayo mauzo ya kila mwaka hayazidi kiwango kilichoainishwa;

(b) kodi ya ongezeko la thamani kwa vyamaa ambavyo mapato yake kwa mwaka hayazidi kiwango kilichoainishwa;

(c) kodi yoyote au ushuru unaotozwa baada ya mauzo au mtaji isipokuwa riba ya mapato, faida, gawio la hisa au kodi inayotokana na uwekezaji wa ushirika nje ya utaratibu wake wa kawaida wa biashara;

(d) ushuru wowote wa mnada unaotozwa kwa mazao ya kilimo na mifugo inayouzwa na / au kwa niaba ya ushirika;
(e) ushuru wowote wa leseni unaotozwa kuhusiana na mauzo ya mtaji; na
(f) ushuru mwingine wowote au ushuru unaofanana na zilizotajwa katika aya (c), (d) na (e) hapo juu.

**Ibara ya 47: Utatuzi wa migogoro**
(a) Mgogoro ni kutoelewana kunakoweza kuathiri biashara ya ushirika kwa namna ambayo husababisha hasara au kuathiri uendeshaji wa chama.
(b) Matumizi ya mbinu mbadala za kutatua migogoro
Migogoro yote itaelekezwa kwanza kwenye upatanishi na ussuluhishi. Mgogoro ambao hauwezi kutatuliwa kwa njia ya upatanishi na usuluhishi utapelekwa kwenye usuluhishi chini ya mwongozo wa mamlaka ya udhibiti wa vyama vya ushirika. Pale ambapo usuluhishi unashindikana, wahusika wanaweza kukimbilia mahakama za sheria zenye mamlaka husika.
(a) Vyama vya ushirika vinajitahidi kushughulikia migogoro kwa kuizuia, kuisshughulikia na kutatua migogoro kwa njia ya onyo la mapema, majibu ya mapema na diplomasia ya kuzuia.
(b) Shirikisho la kitaifa litakuwa na wajibu wa kusuluhisha migogoro katika ushirika na linaweza kuanzisha Vituo vya Usuluhishi vya Ushirika.
Migogoro itatatuliwa kwa taratibu hizo, isipokuwa migogoro ambayo imeweka taratibu za kisheria kama vile migogoro ya ardhi na kazi.

(1) Inapobidi, kutaundwa chombo huru kwa ajili ya kutatua migogoro ya vyama vya ushirika.
(2)

**Ibara ya 48: Makosa ya jinai**
Pale ambapo shughuli ya jinai inafanywa katika ushirika, sheria na taratibu husika za makosa ya jinai zitatumika.

**Ibara ya 49: Chombo cha Udhibiti wa Ushirika**
(1) Kuanzishwa
Mamlaka ya udhibiti wa vyama vya ushirika ambayo itakuwa na jukumu la kudhibiti vyama vya ushirika imeanzishwa, ili kuhakikisha uzingatiaji wa sheria zilizopo za ushirika.
(2) Majukumu ya mamlaka ya serikali inayohusika na vyama vya ushirika:
Majukumu ya mamlaka ya udhibiti yatakuwa:
(a) Kusajili na kufuta usajili wa vyama vya ushirika
(b) Kutoa ushauri wa kitaalamu na kusaidia vyama vya ushirika kuhusiana na uundaji, usimamizi, uandaaji na uendeshaji wa vyama vya ushirika;
(c) Kusimamia utekelezaji wa sera ya maendeleo ya ushirika;
(d) Kutunza na kusambaza taarifa zinazohusiana na maendeleo ya ushirika kwa wahusika wakuu na wadau;
(e) Kutunza daftari la vyama vya ushirika;
(f) Kutunza kanzidata (database) za mambo mbalimbali yanayohusu vyama vya ushirika;
(g) Kukagua na kusimamia vyama vya ushirika;
(h) Kuhimiza na kuhimiza uanzishwaji wa vyama vya ushirika vyenye uhai; na
(i) Kusimamia udhibiti wa vyama vya ushirika ikiwa ni pamoja na sheria ndogo

**Ibara ya 50: Kujidhibiti kwa vyama vya ushirika**
Vyama vya ushirika vitaweka mifumo na taratibu za kuhakikisha na kuwezesha kujidhibiti ili kuongeza/kusaidia mfumo uliopo wa udhibiti wa serikali.

**Ibara ya 51: Mamlaka ya kutunga sheria/kanuni**
Mamlaka ya serikali inayohusika na vyama vya ushirika itakuwa na uwezo wa kutunga kanuni chini ya Sheria hii kwa ajili ya utekelezaji wa Sheria hii. Kanuni zitakazotungwa zitalenga kutoa taarifa za kiutendaji na za kina juu ya utekelezaji wa masharti ya Sheria na zisiwe tofauti na malengo ya Sheria hii.

## SEHEMU YA III
## MASHARTI MENGINEYO

**Ibara ya 52: Tafsiri ya Sheria**
(a) Sheria hii, haraka iwezekanavyo, itatafsiriwa katika lugha inayoeleweka zaidi na inayotumiwa na watu.
(b) Inapobidi matoleo ya Sheria yatatayarishwa na kutolewa kwa umma, wanachama wa vyama vya ushirika na wadau wengine kama mkakati wa kujenga uelewa wa pamoja wa Sheria na mwelekeo wake na falsafa na kanuni ambazo vyama vya ushirika vinafanya kazi.
(c) Sheria hii itapatikana pia kwa lugha ya alama.

**Ibara ya 53: Masharti ya kufutwa na ya mpito**
(a) Pale ambapo Sheria hii na sheria nyingine yoyote ndogo iliyotungwa chini yake itafutwa, vitendo vyote vilivyofanywa hapo awali chini ya Sheria iliyofutwa vitabaki kuwa halali.
(b) Serikali itahakikisha kwamba mipango inayofaa ya mpito inawekwa kabla ya Sheria mpya kuanza kutumika.

**Ibara ya 54: Maandiko Sahihi**
(a) Sheria hii ya Muundo imeandikwa katika lugha zote za kazi za Umoja wa Afrika, na zote ni sawa.
(b) Kukitokea mgogoro, toleo la Kiingereza litatumika kama rejeo.

**Imeidhinishwa Midrand, Afrika ya Kusini,**

**06 Juni 2024**